

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA AROBAINI**

**30 MEI, 2018**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI – TAREHE 30 MEI, 2018

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**331. MHESHIMIWA CATHERINE NYAKAO RUGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-  
Pamekuwa na wimbi kubwa la ukosefu wa ajira kwa sasa huenda kuliko wakati mwingine wowote tangu nchi yetu ipate Uhuru, wahitimu wa tangu mwaka 2015 hawajaajiriwa na Serikali mpaka sasa, Sekta binafsi nazo kila kukicha zinapunguza Wafanyakazi na kutoajiri wapya:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kuhakikisha ajira zinapatikana kwa Vijana hawa ambao hawajapatiwa elimu ya kutosha ya kujiajiri.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**332. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe (Nansio) inakabiliwa na msongamano wa Wagonjwa; Mwaka 2002 Halmashauri ya Wilaya ilitumia zaidi ya Tshs. milioni 200 kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Nakutunguru kama njia ya kupunguza msongamano huo. Hata hivyo ujenzi huu haujakamilika kutokana na ukosefu wa fedha:-

Je, Serikali ipo tayari kuondoa mapungufu yaliyopo ili Kituo hicho kianze kutoa huduma.

**333. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kata ya Bukene Wilayani Nzega inaundwa na Kijiji kimoja tu chenye

wakazi zaidi ya 7,600 jambo ambalo linakwamisha uharakishaji wa huduma za maendeleo kwa Wananchi. Tulishafuata taratibu zote za kuomba Kijiji cha Bukene kigawanywe ili kupata Kijiji kingine kipya:-

Je, Serikali haioni kuwa si sahihi kuwa na Kata inayoundwa na Kijiji kimoja.

**334. MHESHIMIWA EDWIN MGANTE SANNDA (KONDOA MJINI):**

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Pamoja na kuhudumia Wagonjwa wengi wakiwemo watokao Wilaya ya Kondoa, Chemba, Kiteto, Babati na wakati mwingine hata Hanang' lakini Hospitali ya Mji wa Kondoa haina gari la Wagonjwa (*Ambulance*) na uhitaji wa huduma za dharura na rufaa umeongezeka sana baada ya kukamilika kwa barabara kuu itokayo Dodoma – Babati:-

Je, ni lini Serikali itaipatia gari la Wagonjwa Hospitali hiyo.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**335. MHESHIMIWA SAADA SALUM MKUYA (WELEZO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):- Kati ya mambo yaliyokubalika katika mkakati wa kutatua changamoto za Muungano ni pamoja na kugawana ajira zilizopo katika Taasisi za Muungano kwa asilimia 21 (Zanzibar) na asilimia 79 (Tanzania Bara):-

Je, ni kwa kiasi gani mkakati huo umetekelezwa.

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**336. MHESHIMIWA RUKIA KASSIM AHMED (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Lengo la Serikali ya Awamu ya Tano ni kujenga Uchumi wa Viwanda ifikapo 2025:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwavutia Wawekezaji wa Viwanda nchini.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**337. MHESHIMIWA SILVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya TAMCO – Mapinga kupitia Kata ya Pangani ilichukuliwa na TANROADS takribani miaka nane (8) iliyopita:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kujenga barabara hiyo.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**338. MHESHIMIWA ABDUL-AZIZ MOHAMED ABOOD (MOROGORO MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Kuna mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi na Wananchi kwenye mipaka katika Kata za Kauzani na Luhongo ambapo

Wananchi wanashindwa kufanya shughuli zao za maendeleo hasa kilimo kwa sababu Jeshi linaweka mipaka na kuingiza ndani ya mashamba ya Wananchi wakati miaka yote maeneo hayo yalikuwa nje ya mipaka ya Jeshi:-

- (a) Je, ni lini Serikali itawarudishia Wananchi maeneo yao ya kilimo;
- (b) Je, kwa nini Serikali isichukue hatua kwa kuruhusu Wananchi wamiliki maeneo hayo ambayo ni ya asili na Jeshi limewakuta Wananchi katika eneo hilo.

**339. MHESHIMIWA SALUM MWINYI REHANI (UZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Kambi za Jeshi za Ubago na Dunga zinawanyanyasa Wananchi wa Shehia ya Kidimi kwa kuwataka waondoke katika maeneo hayo ambayo ni ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa zaidi ya miaka 40 na wameanza kupima na kuweka bikoni:-

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya hali hiyo, na hatma ya Wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo.

## **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

### **340. MHESHIMIWA PHILIPO AUGUSTINO MULUGO (SONGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

- (a) Je, ni nini mpango wa Serikali kuhusu Ziwa Rukwa hasa kwa kuzingatia kudumaa na kukosekana kwa zao la samaki katika Ziwa hilo;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza bonde la Ziwa Rukwa hasa katika Kilimo cha Umwagiliaji.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
30 MEI, 2018**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**